Kuomba Na Kufunga – Utangulizi wa Uhuishaji wa Utakatifu

Maandiko: Yoeli 2:12-17

Mahubiri haya yanaonyesha kuwa uhuishaji wa utakatifu ni jibu kutoka kwa Mungu baada ya maombi na kufunga kwa kweli kwa watu Wake. Huu unafaa kuwa msukumo kwa Wanazareti katika eneo la Afrika ili kutilia maanani wajibu wetu wa kujitoa nafsi katika maombi na kufunga.

Kumbuka: Muhubiri anafaa kutumia kifungu hiki kama utangulizi.

Utangulizi:

Jeshi la zinge na ukame zitaangamiza Yerusalemu na Yuda. Nabii Yoeli anaona janga hili kuwa ishara ya kuwa siku ya Bwana inakuja" Yoeli 2:31) Hata wakati wa shida alitangaza toba kwa kila mtu, wazee kwa vijana (1:2-3), walevi (1:5), wakulima (1:11) na makuhani (1:13) Hapa zinge wanazungumziwa kama jeshi la Bwana, kuonyesha siku ambayo Israeli itahukumiwa kwa dhambi zake. Kupitia kwa Nabii wake Mungu anaahidi urejesho na Baraka zitafuata hukumu hii ikiwa Israeli itabutu kwa uaminifu.

Dhambi Huleta Hukumu

Wana wa Yuda waliasi Mungu wao:

Mungu anawaita wamrudie (2:12,13).

Walilala na kusahau kulinda maisha yao ya kiroho (1:3)

Walizitimiza tamaa zao za mwili vyema kuliko jinsi walivyotunza maisha yao ya kiroho.

a) Waliitwa "walevi" na "wanywaji wa mvinyo" (1:3)
b) Starehe zao zilitangulia jinsi walivyojitoa kwake Mungu

b. Mungu alihukumu Yuda na Yesusalemu kwasababu ya kutokuwa waaminifu.

Mungu alituma jeshi la zinge kuharibu nchi (2:11)

Ghala zimeachwa katika uharibifu (1:16, 17)

Furaha na shangwe zimetoka kwa nyumba ya Mungu wetu (1:16)

Vijito vya maji vimekauka (1:20)

c. Hukumu hufata dhambi

Sheria ya Agano la kale ya Baraka na Laana (Kumbukumbu la Torati 11:26-28)
Sheria ya Agano mpya ya Dhambi na Hukumu (Warumi 6:23)

d. **Mifano ya Dhambi na Hukumu**

Mifano ya ishara ya hukumu takatifu katika kanisa la jumuia.
Mifano ya dhambi zilizoenea kanisani na katika jumuia.

Mchungaji anafaa kuzitambua dhambi hizi bila kutaja majina ya watu ama hali zo zote.

3) Ukosefu wa neema ya Mungu Kanisani.

e. Tahadhari dhidi ya hatari ya dhambi ikiwa haitashughulikiwa vyema.

2**. Wito kwa Toba kwa njia ya Maombi na Kufunga (2:12-17)**

a. Toba ya jumuia
   1) Nirudieni kwa mioyo yenu yote (2:13, 13)
   2) Toba inafaa kufanywa ya uaminifu na kimoyomoyo, “Rarueni mioyo yenu na siyo mavazi yenu yote. (2:13)

   a) Mchungaji anafaa kutoa baadhi ya mifano ya toba za nje na kueleza jinsi kifungu kinavyokashifu aina hii ya toba.

b. Maombi ya jumuia

Kumlilia Mungu (1:14)

Mrudieni Mungu kwa mioyo yenu yote (2:12)

Wito kwa kubombolewa…..: Wahurumie watu wako ee Bwana” (2:17)

Kuwaleta pamoja watu wa Mungu katika maombi kwajili ya kibali na uwepo wa Mungu.

a) Liiteni kusanyiko takatifu (1:14; 2:25, 16)
b) Iteni wazee na wote waishio katika nchi (1:14)
c) Jumlisheni watoto na hata bwana na bibi arusi watoke chumbani (2:16)

5) Sala Inastahili kuwa njia ya kumtafuta Mungu na wala sio njia ya kujitafutia sifa (Mathayo 6:1-14)

c. Kufunga kwa jumuia

Tangazeni saumu takatifu liiteni kusanyiko takatifu (1:14; 2:15)

Kumbuka kwamba maagizo ya kibiblia katika kifungu hiki ni kwa watu wote ya kujitolea katika kuomba na kufunga. Tumia maandiko yaliyonukuliwa katika B4 hapo awali kwa kusanyiko lote la kidini ili wafunge na kuomba vile vile.

Kufunga (inayoandamana na kumtolea moya) ni ishara ya toba na unyenyekevu, na pia huonyesha kumtegemea Mungu kikamilifu. (Mathayo 6:16-18)

3. Jibu la Mungu Kwa Maombi Kweli ya Toba na Kufunga

Mungu abadilisha Laana na kuifanya Baraka (2:13 na Mambo ya Nyakati 7)

Mungu anaona wivu na kuwalinda watu Wake (2:18, 25)
Mungu anatimiza kila hitaji la watu Wake wanapomgeukia (2:19, 26)

Mungu anatoa uwepo Wake kwa watu Wake (2:28 – 32; 3:21)

Ni muhimu kutia maanani jinsi mstari 2:12 na 3:28 zinavyoanza.
2:12 – “Hata sasa” - (asema Bwana nirudieni kwa kutubu, kufunga na kuomba ni SASA)

2:28 – “Baadaye” - Baadaye nitamimina Roho Yangu juu ya wote

Mungu ametuahidi ikiwa tutamtafuta kwa moyo wetu wote, nasi Tutampata (Mathayo 5:6, 7; Luka 11:15-13).

f. Kumbuka kwamba Petro ananukuu kifungu hiki wakati wa pentekosti, anasema, yale yanayofanyika sasa yalitabiriwa na Yoeli katika Yoeli 2:28-32 (Tazama Matendo ya Mitume 2:16-21)

Nabii Yoeli aliongea kuhusu Bwana akimimina Roho Wake ikiwa tutaomba na uaminifu na kwa kufunga.

Mtume Petro anaunganisha ahadi hii ya Yoeli kwa mambo yanayofanyika katika Agano Jipya wakati wa pentekoste.

4. Matumizi ya Ujumbe Katika Kanisa la Leo Afrika

a. Msingi wa lengo na maono yetu kwa Kanisa la Mnazareti Afrika ni kuwa na ushirika wa kibinafsi na uamsho wa utakatifu kwa jumla (kumiminiwa kwa Roho Wake juu yetu).

b. Eneo letu limechukua hatua ya kufufua utakatifu.
c. Maana ya madhumuni yetu hutoka katika kufufua utakatifu.

d. Hitaji letu kuu Afrika ni kupokea mmiminiko wa Roho wa Mungu kanisani.

Tamati:

Makanisani mwetu katika eneo la Afrika, watu wa Mungu vijana kwa wazee, waume kwa wake, kila mshiriki na kila anayehudhuria wanapewa change moto ya kuungana pamoja kwa maomba na kufunga ili kuomba msamaha binafsi na kwa niaba ya kanisa na jumuia letu, na pia kutenga mda wa kumtafuta Mungu kwa mioyo yetu yote.

Wakati wa kipindi cha lenti, kuanzia Jumatano ya majivu tarehe 22 Februari 2012 hadi Jumapili ya pasaka, tarehe 8 Aprili 2012, Makanisa yote ya Mnazareti yatajitoa katika muda wa kuomba na kufunga.

Tumetenga wakati wa kufunza juu ya kuomba na kufunga na hata kutenga siku, nyakati na vyakula vya kufunga ili kila mshiriki wa Kanisa la Mnazareti aombe na kufunga ili Mungu atuletee ufufuo wa utakatifu katika makanisa yote na kwa wanazareti wote katika eneo la Afrika. Tumia mwongozo wa kuomba na kufunga pamoja na kalenda ili kutambua sehemu, watu na mahitaji ambayo mtaombea wakati huu wa kuomba na kufunga).

Waulize Washiriki ikiwa wamejitayarisha kuomba na kufunga kwa ajili ya nafsi zao, kwa niaba ya jamii, nchi, Eneo letu na watu wetu?

Nabii Yoeli katika agano la Kale pamoja na Mtume Petro wa Agano Mpya, wanatulilia leto kwa sauti moja, “Mtafuteni Bwana kwa moyo wenye toba kwa njia ya kuomba na kufunga, naye Atawamiminia Roho Wake Leo, hapa katika eneo la Afrika na ulimwenguni kote!

MAMBO MUHIMU KWA MCHUNGAJI: Toa changamoto kwa kanisa lote katika kufunga kwa mda wa siku tatu. Baini siku za mfungo huu mapema na utangaze leo wakati wa mahubiri.

Kwa wale ambao wanaweza na hawana tatizo la kiafya, wasile wala kunywa (isipokuwa maji) kwa kipindi cha siku tatu.

Wenye matatizo ya kiafya, wabaini njia zingine za mfungo, mfano kufunga chakula cha mchana ama jioni kwa siku katika kipindi hiki cha siku tatu ama kadiri ya uwezo wao.

Nakala imetayarishwa na Kasisi Howie Shute

Ikiwa Watu Wangu

Andiko: 2 Mambo ya Nyakati 7:11-16

Maandiko: 2 Mambo ya Nyakati 7:14

Utangulizi:

Mahubiri haya yanaonyesha kuwa sisi hujitolea sana kwa mambo ambayo tunayapenda mno maishani mwetu. Tutafanya jambo lolote ili kupata vitu ambavyo tunapenda. Basi, hatufai kujitolea zaidi ili kupolea Baraka za Mungu za kiroho na upako maishani mwetu na kanisani? Mahubiri haya yanatuonyesha kunao haya ya ufufuo na pia linatupa changa moto za hali tulizowekewa na Mungu ili kuwepo na ufufuo maishani mwetu na kanisani mwetu leo. Imethibitishwa kuwa kuomba na kufunga ni baadhi ya masharti ambayo yatamfanya Mungu atende wema maishani mwetu, kanisani, katika jumuia na Afrika yote.

Kielelezo cha kufungua

Tumia kielelezo cha jambo moja la kimaisha ambalo linaonyesha jinsi unavyopenda. Kielelezo kifuatacho ni mfano utakaowasilisha aina ya kielelezo ambacho kitatimiza nia ya mahubiri haya.
Mfano: Nilipokuwa katika shule ya upili, nilipenda mchezo wa lacrosee, mchezo ambao kiasili ulichezwa Amerika na Waamerika wenye asili ya kihindi. Hiki kilikuwa ni kitu kizuri zaidi maishani mwangu. Nilitaka kuwa mchezaji bora zaidi katika timu yangu na hata mchezaji aliyebora zaidi katika timu zote zilizoshindana na shule yetu. Nifanya mazoezi zaidi kuliko wachezaji wengine wote katika timu yangu. Nilichukua hakua ya kuunda goli ambayo niliendelea kufanya mazoezi ili kuhakikisha kwamba niliweza vyema wakati wa kufunga. Nilikuwa nikifanya mazoezi hata usiku. Nilitamani tu kuwa bora zaidi. Wakati mwingine sikuudhuria mafundisho darasani siku za shindano ili niweze kufanya mazoezi ilhali wenzangu walikuwa darasani wakisoma. Nilijitolea kufanya lo lote ili kuhakikisha nimetimiza lengo langu la kuwa mchezaji bora zaidi wa mchezo wa lacrosse katika timu yangu ama timu ye yote. Haya yalikuwa ni maisha yangu nilipokuwa katika shule ya upili. Nilijawa ni hisia za kupenda mchezo wa lacrosse.

Bwana amenikumbusha hisia nilizokuwa nazo katika mchezo wa lacrosse na amenipa change moto kuwa na hisia hizo hizo katika mambo ya Mungu. Kwa njia ya kipekee amenipa changamoto kutufuta ufufuo maishani mwangu na kanisani kwa hisia niliyokuwa nayo katika mchezo wa Lacrosse. Ningefanya jambo lo lote ili kuwa bora zaidi katika Lacrosse. Bwana ameniuliza, “Je, uko tayari kufanya nini ili kuona uhuishaji kanisani lote, pia kupokea moto moyoni mwako na katika matembezi ya ukristo?”

Changamoto kwa Wakristo:

Wakristo wafikirie ni kitu gani maishani ambacho wanahisia kuu kwake na kutafakari wanawezaje kujitoa ili kutimiza hisia hii.

Uliza swali: “Je, u tayari kutenda jambo lipi ili kuona uhuishaji maishani mwako binafsi na kanisani?

Katika Mambo ya Walawi 7:14 Mungu ametupa njia ya uhuishaji. Sasa tuchunguze Andiko hili linalotuwasilishia masharti ya Mungu ya uhuishaji.

Usuli wa maandiko:

a) Mfalme Sulemani alikuwa amekamilisha ujenzi wa hekalu. Aliagiza mapambo ya hekalu yaletwa kwenye mahali patakatifu pa Mungu. Hatimaye Sanduku la Agano lililetwe Hekaluni. Utukufu wa Mungu ulijaa hekaluni.

   Makuhani hawakuweza kuingia hekaluni kwasababu uwepo wa Bwani ulikuwepo (2 Mambo ya Walawi 5:13-14)

   Hili ndilo hitaji kuu la kanisa leo, kwamba uwepo wa Mungu utajaa kwenye hekalu letu (kanisani na katika maisha yetu binafsi).

b) Sulemani aomba maombi ya kuliweka wakfu hekalu katika (2 Mambo ya Walawi 6)
   Sulemani anakubali kuwa wana wa Israeli watatenda dhambi.
   Sulemani anaomba Mungu ili awasamehe dhambi zao wanapoomba wakielekeza macho yao hekaluni wanapotubu dhambi zao.
   Basi Sulemani alipokwisha maombi hayo, moto ukashuia kutoka mbinguni, ukatekeza sadaka ya kuteketezwa na dhabihu; utukufu wa Bwana ukaijaza nyumba.

Wanazareti wa kale waliomba ili Utukufu wa Mungu uwashukie maishani mwao na katika ibada zao za pamoja. Kanisa linahitaji moto ushuke tena – kuona Utukufu wa Bwana umo kati yetu.
Kumbuka: Tenga mda wa kuwasiliana na watu hitaji kuu la uhuishaji leo. Wape change moto ya kuutafuta uso wa Bwana katika uhuishaji Afrika kote.

Bwana akamtokea Sulemani na kumjibu ombi la kuwasamehe watu na kuwaletea urejesho nchini mwao. Kwasababu hii ni haja yetu leo, sasa ni vyema tuchambua kwa makini majibu ya Bwana.

3. Ahadi ya uhuishaji:

a. Maelezo ya utaratibu wa uhuishaji: Bwana alipomtokea Sulemani usiku, Alimpa maelezo ya utaratibu wa uhuishaji, akisema: "Ikiwa watu wangu walioitwa watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao."

Ahadi hii ilifanyiwa wana wa Israeli, watu wa Mungu. Hata hivyo, katika kila jambo, watu wa Mungu ndiyo Kanisa. Wale wanaitwa kwa jina lake wanaitwa Wakristo. Ahadi hii ni yetu kama ilivyokuwa ni ya wana wa Israeli miaka iliyopita.

Neno "IKIWA" linaonekana katika mwanzo wa ahadi.

IKIWA tutakula kiasi kinachofaa, na kufanyisha miili yetu mazoezi, tutapunguza uzani. Lakini IKIWA hatutakula vyema na kufanya mazoezi ya mara kwa mara miili yetu itakuwa na uzito mwingi.

IKIWA tutapanda mimea kwa wakati unaofaa, na IKIWA kutanyesha, mavuno yetu yatakuwa tele. LAKINI IKIWA hatutapanda mbegu zetu kwa wakati unaofaa, na mvua isiponyesha, hatutakuwa na mavuno mema.

Hivyo ndivyo ilivyo hata kwetu. IKIWA tutafanya sehemu yetu, Mungu naye atafanya sehemu Yake, LAKINI IKIWA hatutafanya sehemu yetu, Mungu hatafanya sehemu Yake.

"Ikiwa watu wangu walioitwa watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafutauso na kuziacha njia zao mbaya**; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao."**

b. Sehemu ya Mungu – AHADI YA UHUISHAJI

Atasikia maombi yetu.

Atatusamehe dhambi zetu.

Ataiponya nchi yetu (jumuia, taifa, Kanisa).

Hii ni ahadi ya Mungu – Ataturejeshea maisha na kanisa letu, ikiwa tutatimiza masharti aliyotuwekea.

Tunangojea uhuishaji, lakini uhuishaji unatungojea. Uhushaji utatujia ikiwa tutatimiza masharti tuliyowekewa na Bwana.

"Ikiwa watu wangu walioitwa **watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya**; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao."

d. Sehemu Yetu – MASHARTI YA UHUISHAJI:

Kujinyenyekesha, na Kuomba na Kunitafuta uso

Maana ya kunyenyekea: Kujifunza kutegemea; siotaka makuu ama kujidunisha.

Kimsingi hii ni hali ya moyo ambayo hutufanya kuwa duni mbele za Bwana; hali ya kumtegemea Mungu kikamilifu ili kuutafuta uso wa Bwana, tunahitaji kumtegemea kikamilifu.

Watu wa Agano la Kale walitumia kuomba na kufunga kama njia ya kunyenyekea mbele za Bwana na kutafuta kibali Chake.
(Tazama Zaburi 35:13 na Danieli 9:3).
Kanisa la Agano Mpya liliomba na kufunga ili kuutafuta mapenzi na Baraka za Mungu maishani mwao
(Tazama Matendo ya Mitume 14:23)

Tusipokula kwa muda, tunamwambia Bwana kuwa tunamhitaji Yeye zaidi ya starehe na viburudisho vya maisha yetu; lakini kufunga bila toba ni bure.

Toba: Lazima tuziache njia zetu mbaya (yale mambo ambayo hayampendezi Mungu).

Zungungumza kuhusu baadhi ya mambo ambayo hayampendezi Mungu. Mambo ambayo yanafanywa ama hayafanywi katika jumuia na Kanisani, na uwape watu changamoto ya kugeuka na kuyaacha mambo haya na kuwa watiifu kwa Mungu.

Kufunga Kweli ambao kunampendeza Mungu na ambao humsababisha kutenda ni kutoka kwa watu ambao wamegueka kutoka kwa dhambi zao na walio watiifu kwa sheria na njia zake (Tazama Isaya 58)

4. **Kielelezo – Charles Finney – Mwinjilisti wa Amerikani wa karne ya 19 alitumia Mungu wakati ya Mwamko Mkuu wa Pili Amerikani.**

Finney angehubiri kwa upako mkuu wa Roho Mtakatifu.

Katika mikutano ya uhuishaji, alipohubiri watu walisadikishwa na Roho Mtakatifu hata wangekimbia kwenye altari kwasababu walihofu kuwa watakufa ikiwa hawatatubu na kuomba msamaha wa Mungu.

Wakati mmoja alikuwa na mikutano iliyofuata, ambapo alihubiri wakati wa jioni, basi siku moja wakati wa mchana akaamua kutembelea kiwanda kimoja ili kuona baadhi ya vyombo walivyounda humo. Mkurugenzi wa kiwanda, alimpeleka ili kumwonyesha sehemu mbali mbali za kiwanda. Humo wafanya kazi walikuwa na kazi nyingi. Punde mfanyi kazi mmoja mwanamke akamwona, akatoka kwenye kiti alichokalia, akaanguka chini na kulia kwa sauti ambayo ilikuwa ni kama ya mtu aliyehisi uchungu. Wafanyi kazi wenza pia walianguka chini huku wakilia na kutubu dhambi. Wakati huu wote Finney alikuwa hajasema neno hata moja. Lakini upako wa Roho Mtakatifu uliokuwa juu yake ulikuwa wenye nguvu mno hata watu walihisi uwepo wa Mungu alipoingia kwenye chumba. Mkurugezi wa kiwanda alimsihi Finney aseme na wafanya kazi ili awaweke huru kutokana na uchungu waliokuwa nao. Finney aliwahubiria habari za Kristo na kuwahimiza watubu dhambi zao na kumpokea Kristo kama Mwokozi wao. Wafanyi kazi wote wa kiwanda waliokolewa siku hiyo.

b. **Siri Ya Mafanikio Ya Finney.**

Finney anasema katika habari za maisha yake alizoandika yeye mwenyewe kuwa mzee mmoja kwa jina Kasisi Nash alikuwa akiutembelea mji wo wote alionuia kufanya mikutano ya uhuishaji majuma mawili kabla ya tarehe ya kuanza mikutano. Kisha kutafuta Mkristo mmoja ama wawili kutoka mji ule halafu wanaanza maombi. Nash na jeshi lake la waombaji hawakula wala kulala, na

wakati huo walimsihi Mungu ampe Finney upako atakapokuwa akihubiri katika mji ule na hata pia ili Bwana alete uhuisho juu ya watu wa sehemu ile. Finney hangeweza kuhubiria makutano kabla ya Nash kutafuta upako wa Bwana kwa ajili ya ibada zilizokuwa zimeandaliwa. Finney anasema kila wakati Kasisi Nashi alipomtangulia na kuombea upako wa Mungu na Roho wa kweli kuwasadikisha watu waliohudhuria ibada, Roho Mtakatifu alifanya kazi ya ajabu mno. Lakini ikiwa Nash hakumtangulia, mahubiri hayakuwa na nguvu na mambo machache yalitimizwa katika maisha ya kiroho ya hawa watu.

Mungu alifurahia kuomba na kufunga kwa Nashi zaidi kuliko mahubiri ya Finney.

Tamati: Wito wa Kujitolea

Mchungaji anafaa kuwakumbusha Wakristo jinsi wanavyohitaji Utukufu wa Mungu leo. Wape Wakristo changamoto ya kuingia katika kipindi cha kuomba na kufunga kwa ajili ya uhuishaji wa kiroho:

maishani mwao

katika jamii zao

katika kanisa lao la mtaa

katika jumuia lao

katika Kanisa la Mnazareti Eneo la Afrika.

Tumia kalenda ya Maombi katika kipindi hiki, ili kuombea sehemu tofauti tofauti za Afrika na pia mahitaji mbali mbali ya Afrika.

Nakala imetayarishwa na Kasisi Howie Shute